# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 26-2963822
Nukushi: +255 26-2963828
Barua pepe: sg@nbs.go.tz
Tovuti: www.nbs.go.tz

Barabara ya Jakaya Kikwete,
S.L.P. 2683,
Dodoma
**TANZANIA.**

*Unapojibu tafadhali taja:*
Kumb Na: AC 334/376/01/16

**YALIYOJITOKEZA**

Tarehe: 10 Januari, 2022

## FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA KWA MWEZI DESEMBA, 2021

## 1. MAELEZO YA MBINU NA KANUNI ZA UKOKOTOAJI WA FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA

### 1.1 Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za Bei za Taifa (FBT) ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na sampuli wakilishi ya kaya binafsi nchini Tanzania. Kapu linalotumika kukokotoa FBT lina jumla ya bidhaa 383 ambazo bidhaa 132 ni za Vyakula na Vinywaji Baridi, na bidhaa 251 ni bidhaa zisizo za vyakula. Kwa wigo wa kijiografia, FBT zinakokotolewa kwa kutumia takwimu za bei zinazokusanywa kwenye makao makuu ya mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

### 1.2 Mizania za Fahirisi na Kizio

Mizania za Fahirisi za Bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kwenye ununuzi wa bidhaa na huduma katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kwa maeneo ya mijini na vijijini. Matokeo ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Mwaka 2017/18 yalitumika kama chanzo kikuu cha takwimu za uandaaji wa mizania za Fahirisi. Kizio cha Bei cha Fahirisi zilizofanyiwa marejeo kimeboreshwa na kuwa wastani wa bei za mwezi Januari hadi Desemba 2020, na kizio cha Fahirisi ni mwaka 2020.

### 1.3 Makundi ya Bidhaa na Huduma za Jamii

Fahirisi za Bei za Taifa zinatumia mpangilio wa kimataifa wa matumizi binafsi ujulikanao kama COICOP "*Classification of Individual Consumption by Purpose*" wa mwaka 2018. Aidha, Fahirisi za Bei zinatolewa kwenye makundi 13 ya mpangilio wa COICOP, 2018 pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu ambayo yanajumuisha: - Fahirisi za msingi (*core index*); Fahirisi ya nishati, mafuta na huduma za maji; Fahirisi isiyo ya msingi *(Noncore index);* Fahirisi ya huduma; Fahirisi ya bidhaa; Fahirisi ya huduma za elimu na bidhaa zinazoambatana nazo na Fahirisi ya bidhaa zote isiyojumuisha bidhaa za vyakula na vinywaji baridi.

### 1.4 Namna ya Kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Ukokotoaji wa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi za mwanzo unatumia wastani wa jiometria "*geometric mean of Price Relatives*". Kanuni ya Fahirisi ya *Lowe Index Formula* ambayo ni aina ya "*Laspeyres Index Formula*" hutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

## 2. MFUMUKO WA BEI WA TAIFA KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEONGEZEKA KIDOGO HADI ASILIMIA 4.2

**Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Desemba, 2021, (2020 = 100)**

| Na. | MAKUNDI MAKUU YA FAHIRISI | Mizania (Weight) | Desemba, 2020 | Novemba, 2021 | Desemba, 2021 | Badiliko la mwezi mmoja | Badiliko la miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyakula na Vinywaji Baridi | 28.2 | 100.97 | 103.96 | 105.90 | 1.9 | 4.9 |
| 2 | Vinywaji Vikali na Tumbaku | 1.9 | 100.64 | 102.85 | 102.85 | 0.0 | 2.2 |
| 3 | Mavazi na Viatu | 10.8 | 101.10 | 105.46 | 105.65 | 0.2 | 4.5 |
| 4 | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | 15.1 | 101.20 | 104.69 | 105.14 | 0.4 | 3.9 |
| 5 | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | 7.9 | 100.27 | 103.86 | 104.36 | 0.5 | 4.1 |
| 6 | Afya | 2.5 | 100.51 | 103.39 | 103.39 | 0.0 | 2.9 |
| 7 | Usafiri | 14.1 | 99.49 | 104.15 | 105.33 | 1.1 | 5.9 |
| 8 | Habari na Mawasiliano | 5.4 | 100.94 | 102.34 | 102.42 | 0.1 | 1.5 |
| 9 | Burudani, Michezo na Utamaduni | 1.6 | 98.89 | 102.61 | 102.65 | 0.0 | 3.8 |
| 10 | Huduma za Elimu | 2.0 | 100.06 | 101.16 | 101.16 | 0.0 | 1.1 |
| 11 | Migahawa na Huduma za Malazi | 6.6 | 100.72 | 105.67 | 105.71 | 0.0 | 4.9 |
| 12 | Huduma za Bima na Fedha | 2.1 | 100.03 | 100.35 | 100.36 | 0.0 | 0.3 |
| 13 | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | 2.1 | 99.84 | 103.34 | 103.38 | 0.0 | 3.5 |
| **JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE** | | **100.0** | **100.73** | **104.08** | **104.92** | **0.8** | **4.2** |
| **Makundi Mengine Teule** | | | | | | | |
| 1 | Fahirisi za Msingi (*Core Index*) | 73.9 | 100.65 | 104.84 | 105.25 | 0.4 | 4.6 |
| 2 | Fahirisi Isiyojumuisha Fahirisi za Msingi (*Non-Core Index*) | 26.1 | 100.58 | 101.91 | 104.00 | 2.1 | 3.4 |
| 3 | Fahirisi za Nishati, Mafuta na Bili za Maji | 5.7 | 100.52 | 103.96 | 104.96 | 1.0 | 4.4 |
| 4 | Fahirisi za Huduma | 37.2 | 100.21 | 103.69 | 104.03 | 0.3 | 3.8 |
| 5 | Fahirisi za Bidhaa | 62.8 | 100.88 | 104.31 | 105.46 | 1.1 | 4.5 |
| 6 | Fahirisi za Bidhaa na Huduma za Elimu | 4.1 | 100.06 | 103.28 | 103.36 | 0.1 | 3.3 |
| 7 | Bidhaa zote isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Visivyo na Kilevi | 71.82 | 100.64 | 104.12 | 104.54 | 0.4 | 3.9 |

*Tanbihi: Mjumuisho wa makundi madogo ya Fahirisi yanaweza yasiwe sawa na Fahirisi za Bei za jumla.*

### 2.1 Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa Kipimo cha Mwaka

Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali Namba 1 hapo juu linaonesha kuwa, Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Desemba, 2021 umeongezeka kidogo hadi asilimia 4.2 kutoka asilimia 4.1 kwa mwaka ulioishia mwezi Novemba, 2021. Hii inamaanisha kuwa, kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Desemba, 2021 imeongezeka kidogo ikilinganishwa na kasi iliyokuwepo kwa mwaka ulioishia mwezi Novemba, 2021. Fahirisi za Bei zimeongezeka kutoka 100.73 mwezi Desemba, 2020 hadi 104.92 mwezi Desemba, 2021.

### 2.2 Mfumuko wa Bei wa Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi


Mfumuko wa Bei wa Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi kwa mwaka ulioishia mwezi Desemba, 2021 umeongezeka kidogo hadi asilimia 4.9 kutoka asilimia 4.4 kwa mwaka ulioishia mwezi Novemba, 2021. Kwa upande mwingine, Mfumuko wa Bei ambao haujumuishi Bidhaa za Vyakula

na Vinywaji Baridi kwa mwezi Desemba, 2021 umepungua hadi asilimia 3.9 kutoka asilimia 4.0 ilivyokuwa mwezi Novemba, 2021.

## 2.3 Mfumuko wa Bei wa Fahirisi za Msingi (Core Inflation)

Fahirisi za bei za msingi zinaandaliwa kwa kutojumuisha bidhaa za vyakula zisizochakatwa; nishati na bili za maji. Kutojumuisha bei za bidhaa ambazo zina sifa ya kubadilika mara kwa mara kwenye Fahirisi za bidhaa na huduma zote, hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa Watunga Sera. Fahirisi za bei za msingi zinakokotolewa kwa kutumia bei za bidhaa na huduma 297 na mchango wa mizania kwenye Fahirisi zote ni asilimia 73.9. Mfumuko wa Bei wa Fahirisi za Msingi (*Core inflation*) kwa mwezi Desemba, 2021 umepungua hadi asilimia 4.6 kutoka asilimia 4.7 ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia mwezi Novemba, 2021.

**Kielelezo Namba 1: Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Mwezi Desemba, 2020 hadi Desemba, 2021. (2020 = 100)**




*Tanbihi: Fahirisi za Januari – Desemba 2020 zimefanyiwa marejeo kwa kutumia mwaka 2020 = 100*


Kielelezo Namba 1 kinaonesha kuwa, Fahirisi za Bei zimekuwa na mwenendo imara kutoka mwezi Desemba, 2020 hadi mwezi Desemba, 2021. Katika kipindi hicho, Mfumuko wa Bei ulikuwa kati ya asilimia 3.2 kwa mwezi Desemba, 2020 na Machi, 2021 na asilimia 4.2 kwa mwezi Desemba, 2021.

## 3. FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA KATI YA MWEZI NOVEMBA, 2021 NA DESEMBA, 2021

Fahirisi za Bei za Taifa kati ya mwezi Novemba na Desemba, 2021 zimeongezeka kutoka 104.08 hadi 104.92. Kuongezeka kwa Fahirisi za Bei kumechangiwa na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa Fahirisi za Bei ni pamoja na: - mchele kwa asilimia 3.7, mahindi kwa asilimia 5.2, unga wa ngano kwa asilimia 3.4, unga wa mahindi kwa asilimia 3.3, nyama ya ngombe kwa asilimia 2.3, nyama ya mbuzi kwa asilimia 1.6, samaki kwa asilimia 5.3, matunda kwa asilimia 3.7, mbogamboga kwa asilimia 2.3 na viazi kwa asilimia 3.2. Kwa upande mwingine, baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa Fahirisi za Bei ni pamoja na: - vifaa kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za makazi kwa asilimia 5.0, gesi kwa asilimia 2.3, mafuta ya taa kwa asilimia 1.7, dizeli kwa asilimia 6.7 na petroli kwa asilimia 3.0.

# 4 WASTANI WA MFUMUKO WA BEI WA TAIFA KWA MWAKA 2021


**Kielelezo 2: Mienendo ya Wastani wa Mfumuko wa Bei kwa Makundi Teule ya Bidhaa kwa Mwaka 2020 na 2021**




Kielelezo Na. 2 kinaonesha, kwa ujumla, wastani wa Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwaka 2021 (kutoka mwezi Januari hadi Desemba, 2021) umeongezeka kidogo hadi asilimia 3.7 kutoka wastani wa asilimia 3.3 ilivyokuwa mwaka 2020 (kutoka mwezi Januari hadi Desemba, 2020). Kuongezeka kwa wastani wa Mfumuko wa Bei wa Taifa kumechangiwa na kuongezeka kwa Mfumuko wa Bei wa Bidhaa za Msingi *(Core Inflation)* ambao umeongezeka hadi asilimia 4.1 mwaka 2021 kutoka wastani wa asilimia 2.3 ilivyokuwa mwaka 2020.

Wastani wa Mfumuko wa Bei wa Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi umepungua hadi asilimia 4.2 mwaka 2021 kutoka asilimia 4.8 ilivyokuwa mwaka 2020. Vile vile wastani wa Mfumuko wa Bei wa Bidhaa zote isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi kwa mwaka 2021 umepungua pia hadi asilimia 3.5 kutoka asilimia 3.7 ilivyokuwa kwa mwaka 2020. Wastani wa mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa makundi mengine teule kwa mwaka 2021 ikilinganishwa na mwaka 2020 yana mwenendo wa kushuka kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 2.

**Kielelzo Na. 3: Mwenendo wa Jumla wa Mfumuko wa Bei kwa Mwaka; 2020 na 2021**



Kielelezo Na. 3 kinaonesha kuwa kwa wastani Mfumuko wa Bei wa Taifa umekuwa na mwenendo imara katika kipindi chote cha mwaka ambapo kiwango cha chini kabisa kilikuwa asilimia 3.2 mwezi Machi, 2021 na kiwango cha juu kabisa kilikuwa asilimia 4.2 mwezi Desemba, 2021. Kwa upande wa mwaka 2020, kiwango cha chini kabisa kilifika asilimia 3.0 mwezi Novemba 2020 na kiwango cha juu kabisa kilifika asilimia 3.7 mwezi Januari na Februari, 2020. Kwa maelezo hayo, mwenendo wa Mfumuko wa Bei wa Taifa bado upo ndani ya malengo (Inflation Targets) ya ndani ya Serikali ya kiwango cha asilimia 5.0 ambacho kitakwenda sambamba na makadirio ya ukuaji wa uchumi. Aidha, kiwango cha Mfumuko wa bei nchini cha wastani wa asilimia 3.7 pia kipo ndani ya malengo (Inflation Targets) ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ya asilimia 8.0 na nchi za SADC ambapo ni kati ya asilimia 3.0 hadi 7.0. Hivyo, bado Tanzania inafanya vizuri kwa upande wa uthibiti wa bei za bidhaa na huduma za jamii.

**Jedwali Namba 3: Ratiba ya Utangazaji Fahirisi za Bei za Taifa kwa Miezi Ijayo.**

| Fahirisi za Bei za Taifa | Tarehe ya Toleo |
|---|---|
| Januari, 2022 | 08 Februari, 2022 |
| Februari, 2022 | 08 Machi, 2022 |
| Machi, 2022 | 08 Aprili, 2022 |

**Kwa mawasiliano zaidi kuhusu mbinu za kanuni za ukokotoaji wa Fahirisi za Bei za Taifa na maelezo yoyote yanayohusiana nazo tafadhali wasiliana na: -**

Mtakwimu Mkuu wa Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Takwimu,
Barabara ya Jakaya Kikwete,
S.L.P. 2683,
Dodoma,
TANZANIA.

Simu: +255 26 -2963822,
Nukushi: +255 26 -2963828,
Barua pepe: sg@nbs.go.tz;
Tovuti: www.nbs.go.tz.